## ZOEZI LA KUWEKA WAZI DAFTARI LA AWALI LA MPIGA KURA

### 1.0 Utangulizi

Zoezi la kuweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura ni zoezi lililopo Kisheria kwa mujibu wa Kifungu cha 11A cha Sheria ya Uchaguzi Sura 343. Zoezi hili lengo lake kuu ni kusahihisha kasoro zote zilizopo kwenye Daftari la Awali kabla ya kuchapishwa Daftari la mwisho la Wapiga Kura litakalotumika katika Uchaguzi Mkuu. Zoezi hili litafanyika mikoa yote pamoja na Zanzibar ambapo zoezi la Uandikishaji Wapiga Kura limekamilika na taarifa zake kuchakatwa.

### 1.1 Ratiba ya Kuweka Wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura

Display ya Daftari kwa Mikoa yote itafanyika kuanzia tarehe 7/08/2015 isipokuwa Dar es Salaam na Pwani. Hivyo matangazo ya uhamasishaji yanaweza kuanza kutolewa kuanzia tarehe 04/08/2015.

### 1.2 Matumizi ya Daftari la Awali

Madaftari yaliyochapishwa yatatumika pia katika udhamini wa Wagombea hivyo kama ilivyofanyika katika chaguzi zilizopita kurasa za Daftari lililochapishwa hazitabandikwa katika kuta au mbao za matangazo bali zitabaki katika vitabu vyake na Wapiga kuwa watakabidhiwa Daftari kama lilivyochapishwa na kulikagua. Haita ruhuriwa kuchana kurasa yeyote katika Daftari.

### 2.0 Sura ya Daftari

Daftari la Awali la Wapiga Kura limegawanyika katika sehemu kuu tatu:-

i. **Sehemu ya Kwanza (cover page)**: ambayo huonyesha mipaka ya kiutawala ambayo ni Mkoa, Halmashauri, Jimbo, Kata, Kijiji/Mtaa na kituo cha kujiandikishia. Pia huonyesha tarehe ya kuchapishwa kwa Daftari, idadi ya Kurasa na Idadi ya Wapiga Kura waliomo kwenye Daftari husika

ii. **Sehemu ya pili**: Sehemu hii huchapishwa taarifa za Wapiga Kura wenye sifa ya kuwa Wapiga Kura

iii. **Sehemu ya tatu:** Sehemu hii huchapishwa taarifa Wapiga Kura waliojiandikisha lakini baada ya kuchakata taarifa walibainika kukosa sifa ya kuwa Wapiga Kura hivyo kuondolewa katika Daftari la Wapiga Kura. Huonyesha pia sababu iliyofanya kukosa Sifa mfano Kujiandikisha zaidi ya maramoja, siyo raia wa Tanzania, kifo, umri chini ya miaka 18, kuhukumiwa kifungo zaidi ya miezi 6.

**3.0 Zoezi la kuweka wazi Daftari**

Zoezi la kuweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura linalenga kuondoa kasoro mbalimbali zilizojitokeza wakati wa Uandikishaji hivyo kufanya Daftari kuwa sahihi na la kuaminika. Katika zoezi hili Wapiga Kura hutakiwa kuangalia usahihi wa taarifa zao baada ya kuchakatwa ikiwa ni pamoja na mambo yafuatayo:-

i. Kusahihisha kasoro zozote zilizo katika taarifa za Mpiga Kura mfano jina, jinsia, tarehe ya kuzaliwa, n.k.
ii. Kuangalia iwapo taarifa za Mpiga Kura aliyejiandikisha zipo katika Daftari
iii. Kuweka pingamizi kwa Jina au taarifa za Mpiga Kura asiye na Sifa ya kuwepo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Mambo yanayomwondolea Mpiga kura Sifa ya kuwa Mpiga Kura ni pamoja na Uraia wa mtu aliyejiandikisha kuwa Mpiga Kura, Kifo, Kifungo zaidi ya miezi sita, kuwekwa kizuizini kwa amri ya Rais, kutenda makosa ya kiuchaguzi, kuthibitishwa kuwa Mpiga Kura aliyejiandikisha hana akili timamu, kuwa na umri chini ya mika 18 ifikapo siku ya Uchaguzi na kujiandikisha zaidi ya mara moja ambapo sehemu nyingine hutakiwa kuondolewa katika Daftari.
iv. Kurekebisha mipaka ya kiutawala (delimitation structure)
v. Kuangalia kama idadi ya Wapiga Kura inayoonyeshwa kwenye Daftari ni Sahihi
vi. Kuhamisha taarifa za Mpiga kura aliyehama kutoka Kata, Jimbo moja kwenda Kata, Jimbo jingine
vii. Kutoa kadi kwa Wapiga Kura waliopoteza kadi zao.
viii. Kutoa vitambulisho kwa Wapiga kura walioandikishwa kwenye mfumo wa mafunzo.

**4.0 BVR Kits zitakazotumiwa katika Zoezi la Display**

Zoezi la Uandikishaji limefanyika muda mfupi uliopita hivyo inategemewa hakutakuwa na Wapiga Kura wengi waliopoteza kadi au waliohama kutoka kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine. Kutokana na sababu hii Tume itaweka BVR Kit mbili (2) katika Halmashauri kwa ajili ya wale tu waliopoteza kadi zao au wale wanaohitaji kubadilisha kadi zao za kupigia kura iwapo zina kasoro. Zoezi hili halihusishi Uandikishaji wa Wapiga Kura wapya

Zoezi la uwekaji Daftari Wazi katika Kata litafanyika kwa siku tano (5) kuanzia saa mbili asubuhi(2:00) mpaka saa kumi na mbili jioni (12:00) katika ngazi ya Kata. Kila Kata itakuwa na Madaftari ya Vituo vyote vilivyopo katika Kata husika.

Idadi ya taarifa za Wapiga Kura zilizorekebishwa mfano jina, tarehe ya kuzaliwa, jinsia, waliopoteza Kadi, waliohama, waliofariki, waliojiandikisha zaidi ya maramoja na kuchukuliwa hatua za kisheria n.k zinatakiwa kuletwa Tume haraka iwezekanavyo.

Taarifa za Wapiga Kura waliopingwa kuendelea kuwemo kwenye Daftari la Wapiga ambao wamekata rufaa katika mahakama za Wilaya ziletwe Tume zikionyesha idadi na Mahakama na Hakimu aliyepangiwa kusikiliza shauri hilo. Hii itarahisisha Tume kufuatilia na kurekebisha Daftari mapema kulingana na Hukumu ya Mahakama. Idadi ya taarifa zilizorekebishwa ziletwe Tume

Wapiga kura watakaokosa taarifa zao kwenye Daftari la Wapiga Kura lakini wana kadi za kupigia kura wataandikishwa upya kwa kutumia fomu namba 1 na kupewa kadi nyingine na watatakiwa kurudisha kadi walizopatiwa katika uandikishaji kwani Kadi mya itakuwa na namba mpya. Namba ya kadi mpya ndiyo itakayokuwa namba ya kudumu. Watakaoandikishwa upya wanatakiwa kuchukuliwa upya picha, alama za vidole, saini, na taarifa zao.

## 5.0 Wapiga Kura waliojiandikisha zaidi ya Mara Moja

Kujiandikisha zaidi ya mara moja **kwa makusudi** ni kosa la Jinai. Baada ya zoezi hili la kuweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura, orodha ya majina ya Wapiga Kura waliojiandikisha zaidi ya mara moja pamoja na picha zao, itakabidhiwa kwa Afisa Mwandikishaji (RO). Afisa mwandikishaji, baada ya kuichunguza orodha hiyo na kujiridhisha kuwa kuna Wapiga Kura waliojiandikisha zaidi ya mara moja **kwa makusudi**, orodha hiyo ataiwasilisha polisi kwa hatua zaidi za Kisheria. Mpiga Kura ataachiwa kadi moja tu na kukabidhi nyingine kwa Afisa Mwandikishaji ili aziwasilishe Makao Makuu ya Tume. Aidha taarifa kamili ya Kadi walizoachiwa Wapiga Kura ziwasilishwe Tume mapema.

Afisa Mwandikishaji atatakiwa pia kufuatilia mwenendo wa Kesi na iwapo Mpiga Kura alityejiandikisha zaidi ya mara moja atafungwa zaidi ya miezi sita atajaza Fomu Na. 5B na taarifa zake ziwasilishwe Tume mara moja.

## 6.0 Daftari la Awali kutumika katika Udhamini wa Wagombea

Wagombea katika chaguzi za Rais, Bunge na Madiwani hutakiwa kudhaminiwa na Wapiga Kura. Kwa Mpiga Kura aliyejiandikisha na kupatiwa Kadi Mpya ataweza kumdhamini Mgombea. Daftari hili la Awali litatumiwa na Afisa Mwandikishaji kuhakiki Wapiga Kura watakaowadhamini wagombea wao kwani Mpiga Kura asiye na sifa hataweza kumdhamini mgombea. Wapiga Kura wataakiwa kuhakiki taarifa zao kabla ua

kumdhamini Mgombea au Kabla ya Uchaguzi ili kupunguza au kuondoa kabisa malalamiko siku ya Uchaguzi.

## 7.0 Uhakiki wa Taarifa

Katika kurahisisha uhakiki wa taarifa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeweka Mfumo utakaowarahisishia Wapiga Kura kukagua taarifa zao. Mfumo huu umekuwa ukitumika tangu mwaka 2005 na Umetumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Mfumo huu **SIYO MFUMO WA UPIGAJI KURA NA HAUNA UHUSIANO NA UPIGAJI KURA** kwani Upigaji wa Kura utafanyika kama chaguzi zilizopita kwa kutumia Karatasi za Kura (Ballot Paper) ambazo huesabiwa katika Vituo vya Kupigia Kura (Polling Stations) na matokeo yake kubandikwa katika Vituo hivyo vya Kupigia Kura.

Mfumo unamwezesha Mpiga Kura kuhakiki taarifa zake au kujua kituo chake cha kupigia kura popote Mpiga Kura alipo badala ya kwenda katika Ofisi za Kata kufanya Uhakiki. Mpiga Kura mwenye simu ya aina yeyote au anayeweza kutumia Tovuti ataweza kuhakiki taarifa zake mahali popote atakapokuwa kwa njia zifuatazo.

- Ujumbe mfupi kwa njia ya simu (SMS)
- Tovuti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi

## 7.1 UJUMBE MFUPI KWA NJIA YA SIMU YA MKONONI (SMS)

Njia hii ni ya kutumia simu za Mkononi (Cellular Phones). Mpiga Kura ataingiza namba iliyochapishwa katika Kadi yake ya kupigia kura katika simu na taweza kuhakiki taarifa zake. Maelekezo ya kutumia njia ya SMS kuhakiki taarifa ni kama ifuatavyo;

I. Bonyeza namba *152*00#

II. Chagua namba 2 inayoonyesha "Uchaguzi mkuu 2015"

III. Baada ya hapo chagua namba (1) Kuhakiki taarifa au namba (2) kutoa taarifa ya kitambulisho chenye kasoro

IV. Iwapo namba 1 itachaguliwa yaani uhakiki wa taarifa, utatakiwa kuingiza namba ya iliyochapishwa katika Kadi ya Mpiga Kura bila kuandika T au alama (-) mfano T-1001-2692-028-9 itaandikwa 100126920289 hivyo bonyeza kitufe reply ili kuingiza namba hiyo

V. Baada ya hatua hiyo utatakiwa kuingiza namba 1 kukubali au namba 2 kughahiri

VI. Ukichagua namba (1) Ujumbe utapelekwa katika Mfumo na utapatiwa ujumbe wa kusubiri taaarifa zako iwapo zipo katika Daftari. Ukichagua namba 2 utaondoka katika Mfumo.

VII. Iwapo Upo katika Daftari taarifa zako zitarudishwa kama zilivyoingizwa katika Daftari hivyo unatakiwa kuzihakiki kama zipo sahihi. Iwapo zipo sahihi unaweza tu kuondoka katoka mfumo. Iwapo zitakuwa zimekosewa unatakiwa kuonyesha na kwenda katika Kata au Halmashauri yako na kuzirekebisha na kupatiwa kitambulisho kingine wakati wa zoezi la kuweka wazi Daftari.

## 7.2 KWA KUTUMIA TOVUTI YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

Njia nyingine ya kurahisisha uhakiki wa taarifa ni wa kutumia Tovuti. Tovuti ya Tume inakurasa ambayo imeandaliwa kwa ajili ya uhakiki tu wa taarifa za Mpiga Kura. Maelekezo ya njia hii ni kama ifuatavyo:-

I. Ingia katika tovuti ya Tume ambayo ni ***http://www.nec.go.tz.***

II. Nenda katika kurasa ya taarifa za Mpiga Kura

III. Baada ya dirisha la kuingiza namba ya mpiga kura soma maelekezo kwa makini kisha ingiza namba yako ya mpiga kura inayoonekana kwenye kadi yako ya mpiga kura inayoaanzia na T-1001.........

IV. Kama Mpiga Kura ameandikishwa na yupo kwenye Kanzi Data ya Tume, taarifa zake zitarudishwa, kama Taarifa zake hazipo kwenye Kanzi Data ya Tume, utarudishiwa ujumbe kuwa haujaandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga kura.

V. Kila hatua hakikisha unasoma maelekezo kwa makini.

## 8.0 HITIMISHO.

Ikumbukwe kwamba zoezi hili ni la kubaini makosa yaliyojitokeza na pia kuyafanyia marekebisho. Afisa Mwandikishaji ataakiwa kuwahamashisha wananchi wote waliojiandikisha wajitokeze kwa wingii ili kuweza kubaini kasoro zote zinazoweza kulalamikiwa siku ya Uchaguzi. Kasoro zote zitaweza kutatuliwa hivyo kasoro zikibainishwa na zitafanyiwa kazi hivyo kuwa na Daftari lililo sahihi na kuaminika.

Baada ya uwekaji wazi Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kumalizika madaftari yataendelea kutumika katika zoezi la Udhamini na baada ya zoezi hilo madaftari yasitumike kwenye zoezi lolote lingine hata siku ya Uchaguzi, ikiwezekana yateketezwe.